

# TUME YA NGUVU ZA ATOMIKI TANZANIA



## TAARIFA KWA WAMILIKI WA VIFAA VYENYE VYANZO VYA MIONZI NCHINI

Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania inapenda kuwataarifu wamiliki vifaa vyenye vyanzo vya mionzi nchini, kuhakikisha kuwa wana leseni hai ifikapo Julai 1, 2017.

Kwa mujibu wa sheria ya Nguvu za Atomiki Na. 7 ya mwaka 2003, ni kosa kisheria kuingiza, kutumia, kumiliki au kusafirisha kifaa / vifaa vyenye vyanzo vya mionzi bila kuwa na leseni inayotolewa na Tume.

Mtu au Taasisi yeyote itakayobainika kuingiza, kutumia, kumiliki au kusafirisha kifaa / vifaa vyenye vyanzo vya mionzi bila leseni hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mhusika ikiwemo kifungo, faini au vyote viwili kwa pamoja.

Imetolewa na;

**Mkurugenzi Mkuu,**

**Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania,**

**S.L.P 743,**

**Arusha.**

**Simu namba +255 272970050/51/53**

**Barua pepe: official @taec.or.tz**

**Tovuti: www.taec.or.tz**